

Je, unajua kuna vitu vichache kulipia unapokodi miliki katika New South Wales?

Makubaliano mengi ya upangaji au hati nyingi ya kukodisha inahitajika wapangaji kulipa dhamana na kodi chambele.

Kwa hiyo, tuanze na dhamana.

Dhamana ni pesa iliyolipwa na mpangaji kwa ajenti au kabaila na inawekwa kama amana – kama mpangaji anavunja makubaliano ya upangaji.

Dhamana moja tu inalipiwa kwa kila makubaliano ya upangaji hata kama kuna zaidi kuliko mpangaji mmoja katika miliki.

Pesa za dhamana si zaidi ya kodi ya wiki 4 kwa vyovyote kama miliki ina fanicha au haina.

Maajenti au kabaila wengi wataomba kwa dhamana mzima kulipiwa wakati mpangaji anaweka saini kwa hati ya kukuodisha.

Lazima ajenti au kabaila akupe resiti kwa malipo yoyote ya dhamana unayotoa, isipokuwa inaandikwa kwenye hati ya kukodisha.

Pia wamalize kujaze fomu ya Kuweka Dhamana ya Upangaji pamoja na malipo yaliyolipwa.

Fomu hii lazima iwekwa saini na wote wawili mpangaji na kabaila na kupelekwa kwa Fair Trading inayotunza dhamana iliyowekwa.

Mpangaji atapokea notisi ya kuhakikisha na Rental Bond Number kutoka Fair Trading.

Notisi hii lazima itunzwe pamoja na hati ya kukodisha.

Kawaida pesa za dhamana zinarudishwa kwa mpangaji wakati wa mwisho wa makubaliano ya upangaji.

Pengine, maajenti au makabaila wataamua kuomba pesa kutoka dhamana.

Kwa mfano, kabaila anaweza kudai dhamana kama mpangaji ameacha zulia na madoa au uchafu au kama mpangaji hajalipa kodi.

Gharama nyingine ya kwanza kufikiria ni kodi chamebele ya wiki 2.

Hii inalipwa mwanzo wa upangaji.

Baada ya kulipa kodi chamebel ya wiki 2, kodi yako ijayo inahitaji kulipiwa baada ya wiki 2 zaidi kupita.

Kama mpangaji, uwahi kulipa kodi yako. Waweza kupanga kwa njia iliyopanguliwa kulipa kodi yako ili hutachelewa kulipa.

Kwa mfano, pesa za kodi zinaweza kuchukuliwa mara moja kutoka akaunti yako ya benki kwa taraha fulani.

Hakikisha una pesa za kutosha katika akaunti yako ya benki au utalipa ada za benki.

Lazima majenti wakupe chaguo ya njia aina moja ya kulipa bure kama Centrepay, EFTPOS katika ofisi zao.

Kwa hiyo, ni wazo zuri kufahamu kuhusu gharama zote hizo kabla kuweka saini hati ya kukodisha.

Wasiliana na Housing NSW kama ukistahili posha ya Rentstart.

Kwa mabishana ya maombi ya dhamana wasiliana na Fair Trading.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya Fair Trading kwa [www.fairtrading.nsw.gov.au](http://www.fairtrading.nsw.gov.au) au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihitaji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.